# MAJI TANZANIA

TOLEO NA 021

JULAI- SEPTEMBA, 2023

## Serikali kufikisha maji katika kata mbili zilizobaki Kilwa.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amewahakikishiwa wananchi wa kata za Limaliyao na Kivinje jimbo la Kilwa Kusini kuwa serikali inaendelea na jitihada kuhakikisha huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza inafikishwa katika kata hizo.

Amesema hayo katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kilwa Masoko mara baada ya kupokea maombi kutoka kwa Mbunge wa jimbo hilo Mhe. Ally Kasinge ambaye amesema kata hizo bado hazijafikiwa na huduma ya majisafi.





## Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Maji yawasilishwa UN

## Serikali yaahidi kutoa milioni 500 kusambaza maji mjini Lindi

Serikali imeahidi kutoa shilingi milioni 500 ili kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji kwa wananchi wa Lindi Mjini, ahadi hiyo imetolewa na Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) wakati wa ziara ya kikazi ya Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika viwanja vya Mitwero Mjini Lindi.



# “Serikali itaendelea kuwekeza katika sekta ya maji mkoani Mtwara” - Rais Samia

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amezindua mradi wa maji, wa chujio la maji la mradi wa maji wa Mtwara na kuwahakikishia wananchi wa mkoa huo kuwa Serikali itaendelea kuwekeza katika sekta ya maji ili kila mkazi anufaike na huduma hiyo muhimu.

Amesema hayo akizungumza na wananchi katika wa Uwanja wa Nangwanda Sijaona mara baada ya kuzindua mradi huo eneo la Mangamba mjini Mtwara.

Amesema chujio alilolizindua litanufaisha asilimia 80 ya wakazi wa mji wa Mtwara na hivyo kusukuma maendeleo kwa wananchi wa mkoa huo.

Kwa upande wake, Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya maji katika Mkoa wa Mtwara ili kutatua changamoto ya huduma ya maji.

“ Mahitaji ya maji katika mji wa Mtwara ni lita milioni 18 kwa siku ambapo uzalishaji kwa sasa ni lita milioni 14, na kuna upungufu ni lita milioni 4. Aidha, Serikali imetoa bilioni 19 ili kutatua changamoto hiyo” Aweso amesema.

Amewataka wawekezaji mbalimbali katika sekta ya Viwanda kujitokeza mkoani hapo kwani huduma ya maji imeimarishwa kwa kiasi kikubwa.

“Wananchi wa Mtwara niwaeleza kuwa, pamoja na mafanikio tuliyofikia, Mhe. Rais Samia ameridhia na wadau watakwenda kutekeleza ndoto mliyoiomba kwa muda mrefu ya kutumia maji ya mto Ruvuma.” Waziri Aweso amesisitiza.

Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan amefanya ziara ya kikazi mkoni Mtwara, hivi karibuni ambapo amekagua,na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo.










# Rais Samia awapa Mtwara uhakika wa maji

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewahakikishia wananchi wa mkoa wa Mtwara kuwa serikali inaendelea na jitihada mbalimbali ili kuhakikisha wananchi wote wa mkoa huo wanafikiwa na huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza.

Rais Samia ameyasema hayo wakati akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Newala katika uwanja wa Sabasaba mara baada ya kutembelea banda la Wizara ya Maji na kupata maelezo kuhusu mradi wa maji wa Makonde kutoka kwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri.

Amesema mradi wa maji wa Makonde unaotekelezwa mkoani hapo utahudumia sehemu kubwa ya wananchi na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya huduma ya majisafi.

Mhe. Rais Amewapongeza Wizara ya Maji kwa kuendelea kusimamia ili mradi huo ukamilike kwa wakati.

Kabla ya kuwasili wilayani Newala akitokea Mtwara mjini, Mhe. Rais Samia alisimama na kuzungumza na wananchi wa eneo la Nanguruwe, wilaya ya Mtwara, Jimbo la Mtwara Vijijini.

Katika mkutano huo Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) alipata fursa ya kuzungumza na wananchi na kuwahakikishia kuwa serikali imejipanga kwa mipango mizuri ili wananchi wa mkoa wa Mtwara ikiwemo jimbo la Mtwara Vijijini kunufaika na majisafi na salama yenye kutosheleza.

Mipango hiyo ni pamoja na kuhakikisha unatekekezwa mradi mkubwa utakaotumia chanzo cha mto Ruvuma ili kuhudumia maeneo mbalimbali mkoani hapo.







# Serikali kufikisha maji katika Kata mbili zilizobaki Kilwa.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amewahakikishiwa wananchi wa kata za Limaliyao na Kivinje jimbo la Kilwa Kusini kuwa serikali inaendelea na jitihada kuhakikisha huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza inafikishwa katika kata hizo.

Amesema hayo katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kilwa Masoko mara baada ya kupokea maombi kutoka kwa Mbunge wa jimbo hilo Mhe. Ally Kasinge ambaye amesema kata hizo bado hazijafikiwa na huduma ya majisafi.

“Mhe. Mbunge maendeleo ni safari. Tumeshaianza safari kwenye kata nyingine, lengo letu ni kuhakikisha hizo kata mbili zilizobaki pia zinafikiwa na huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza”

Rais Samia amesema na kusisitiza kuwa ahadi ya Serikali ni kuhakikisha huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza inamfikia kila Mwananchi.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ameshiriki katika ziara hiyo katika kuhakikisha maagizo na maelekezo yote yanayotolewa na Rais yanatekelezwa kwa wakati na viwango.






Mhandisi Mwajuma Juma Waziri akila kiapo kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji katika hafla fupi iliyofanyika Ikulu ndogo ya Tunguu Zanzibar, tarehe 01 Septemba, 2023.

# Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Maji yawasilishwa UN




Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango amemwakilisha Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano wa Jopo la Viongozi wa Ngazi ya Juu la Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Maji Barani Afrika (Continental Africa Water Investment Programme (AIP) High-Level Panel kilichofanyika tarehe 19 Septemba 2023, jijini New York nchini Marekani.

Makamu wa Rais Mhe. Mpango katika mkutano huo amezungumzia Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Maji nchini Tanzania (Tanzania Water Investment Programme-TanWIP) 2023-2030 yenye bajeti ya Dola za Marekani bilioni 15.02.

TanWIP ni sehemu ya Programu ya Uwekezaji katika sekta ya Maji Barani Afrika inayolenga kuongeza uwekezaji katika Sekta ya Maji kwa wastani wa Dola za Marekani bilioni 30 kwa mwaka.

Mkutano huo umebebwa na kaulimbiu isemayo Mind the Gap: Invest in Water na kufunguliwa kwa pamoja na Mhe.Marky Sall, Rais wa Senegal na Mwenyekiti Mwenza wa Jopo (Co-Chair); Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Global Water Partnership Southern Africa na Mwenyekiti Mwenza Mbadala wa Jopo (Alternate Co-Chair).

Programu ya AIP na TanWIP zinalenga katika kuhakikisha usalama wa maji, uhakika wa huduma za maji na maendeleo ya jamii na uchumi kupitia maji.

## Serikali yaahidi kutoa milioni 500 kusambaza maji mjini Lindi



Serikali imeahidi kutoa shilingi milioni 500 ili kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji kwa wananchi wa Lindi Mjini, ahadi hiyo imetolewa na Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) wakati wa ziara ya kikazi ya Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika viwanja vya Mitwero Mjini Lindi.

Amesema utekelezaji wa mradi wa maji wa Ng'apa umewezesha uzalishaji mkubwa wa maji na hivyo kuimarisha huduma ya maji kwa wananchi wa Lindi.

Mhe. Aweso amekiri kuwepo kwa changamoto ya miundombinu ya usambaji maji kwani mahitaji ya maji kwa watu wa Lindi ni lita za ujazo milioni 7 kwa siku wakati uzalishaji ni zaidi ya milioni 10

"Nimuahidi Dada yangu Hamida Abdallah(Mb), Mbunge wa Jimbo la Lindi mjini kuwa ndani ya wiki hii wizara italeta kiasi cha shilingi milioni 500 ili wananchi wa Lindi wasambaziwe maji" Aweso amesema.

Awali akitoa salamu za wananchi wa jimbo la Lindi mjini Mbunge wa Jimbo hilo Mhe. Hamida Abdalah (Mb) aliomba serikali iwezeshe ujenzi wa miundombinu ya maji kwa wananchi kwani uhitaji ni mkubwa. Mhe. Hamida amepongeza jitihada kubwa zinazofanywa na serikali kuhakikisha wananchi wa jimbo la Lindi wanapata huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza.

# Makamu wa Rais aweka jiwe la msingi la mradi wa maji mkoani Ruvuma



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Phillip Isdor Mpango ameweka jiwe la msingi la ujenzi wa mradi wa maji wa Liuli Group mkoani Ruvuma. Mradi huo una thamani ya shilingi 4,718,087.85.

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) katika hafla hiyo amesema kuwa kazi zilifanyika ni Pamoja na ujenzi wa matanki matatu yenye jumla ya ujazo wa lita 535,000; ulazaji wa bomba la usambazaji maji kwa urefu wa kilomita 58. 5; ulazajiwa bomba kuu lenye urefu wa kilomita 12.9 pamoja na ujenzi wa vituo 19 vya kuchotea maji.

Mhe. Dkt. Mpango, Makamu wa Rais, ameipongeza Wizara ya Maji kwa kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji nchini, na kusisitiza mradi huo uweze kuhudumia wakazi wa Liuli pamoja na maeneo ya pembezoni, pia wananchi washirikishwe katika kuhifadhi vyanzo vya maji.

Utekelezaji wa mradi huu unafanyika kwa fedha kutoka Mfuko wa Taifa wa Maji (NWF) na Serikali kuu.



# Wizara ya Maji yatakiwa kutekeleza mwongozo wa ubia na sekta binafsi

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), amempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu fedha nyingi ambazo zimewezesha utekekezaji wa miradi ya Maji.

Mhe. Majaliwa ambaye pia ni Mbunge wa Ruangwa ametoa pongezi hizo kwa Mhe. Rais Samia katika mkutano wa hadhara kwenye viwanja vya Maonesho Kilimahewa, Ruangwa mjini.

Amesema kupitia Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) zaidi ya shilingi bilioni 184 zilitolewa na kuwezesha utekelezaji wa mradi ambao umehudumia mji mdogo wa Nyangao hadi Ruangwa na hivyo kuwezesha zaidi ya vijiji 55 kupata huduma ya maji.

Amesema Wizara ya Maji imetekekeza miradi mingi na inaendelea na utekekezaji ambao unatoa matumaini kwa wananchi wa Ruangwa.



Ameishukuru Wizara ya Maji kwa usimamizi mzuri wa fedha kwani miradi iliyotekekezwa inathibitisha viwango na ubora unaostahili.



# Mradi wa maji wa milioni 798.7 wazinduliwa Mtwara



Mradi wa maji wenye thamani ya shilingi milioni 798.7 umezinduliwa Tandahimba, mkoani Mtwara na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb).

Mhe. Majaliwa ameipongeza Wizara ya Maji kwa kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji nchini na kusisitiza kuwa wananchi walinde miundombinu ya miradi ya maji pamoja na kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji ili miradi inayotekelezwa iwe endelevu.

Naibu Waziri wa Maji Mhe.Mhandisi Maryprisca Mahundi(Mb) katika uzinduzi huo amesema mradi huo wa majisafi wa Kitama, pamoja na mengine umehusisha, ulazaji wa bomba umbali wa kilomita 20.1 , na ujenzi wa vizimba vya umma vya kuchotea maji 10.

Ameongeza Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa uboreshaji huduma ya maji katika miji 28 ambapo kwa Wilaya ya Tandahimba mkandarasi ameshaanza utekelezaji wa mradi wa maji wa Makonde kwa gharama ya shilingi bilioni 84 na ameshalipwa shilingi bilioni 12 za kuanza utekelezaji



# Waziri wa Maji Aweso amezindua tanki la maji la lita 1,000,000 Mkoani Kagera



Waziri wa Maji Mhe Jumaa Aweso (Mb) amezindua tanki la maji la lita 1,000,000 linalowahudumia wakazi wa Biharamulo mjini, mkoani Kagera.
Sanjari na hilo, amezindua ofisi ya Mamlaka ya Majisafi Biharamulo.
Waziri Aweso pia amekagua na utekelezaji wa mradi wa maji wa Nemba unaotekelezwa na RUWASA, na kufungua ofisi ya Jumuiya ya Watumia Maji ya Nemba.
Akifanya tathmini ya hali ya upatikanaji wa maji ametaka kazi zaidi ifanyike eneo la Nyakaula na Nyakanazi kutokana na ongezeka la idadi ya wakazi ambao wanahitaji huduma ya uhakika ya maji.
Amewataka wakazi wa Biharamulo kuthamini utunzaji wa mazingira na kulinda vyanzo vya maji ili kuwa na uhakika wa huduma ya maji.

Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Mhandisi Ezra Chiwelesa amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kufanikisha upatikanaji wa fedha za miradi mingi ya maji kwa wakazi wa Biharamulo.







Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ameiwakilisha vyema Sekta ya Maji katika tukio laMhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na viongozi pamoja na Wananchi wa Mkoa wa Mtwara katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika uwanja wa Nangwanda Sijaona.



# Kamati ya Bunge yaipa heko Wizara ya Maji

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira imeipongeza Wizara ya Maji kwa kuwa mstari wa mbele katika kusimamia maelekezo mbalimbali ambayo yamekuwa yakitolewa na kamati hiyo. Pongezi hizo zimetolewa leo Jijini Dodoma wakati Wizara hiyo ilipokuwa ikiwasilisha utekelezaji wa shughuli za Chuo cha Maji.

Mhe. Jackson Kiswaga (Mb) Mwenyekiti wa Kamati hiyo amesema Wizara ya Maji imekuwa sikivu katika kufanyia kazi maoni na maelekezo mbalimbali hivyo imeweza kupata mafanikio, ikiwamo maendeleo makubwa katika Chuo cha Maji.

Amesisitiza na kuwataka wahakikishe watumishi wa Sekta ya Maji wanaendelea na utaratibu huo ili kuleta mabadiliko chanya kwa Watanzania.

Awali akiwasilisha taarifa ya chuo hicho kwa niaba ya Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) Mkuu wa Chuo cha Maji Dkt. Adam Karia amesema Chuo cha Maji kimekuwa na mafanikio anuwai ikiwemo ongezeko la watahiniwa pamoja na machapisho ya tafiti mbalimbali ambazo zimekuwa msaada mkubwa katika kukuza uchumi na kutoa majibu ya changamoto mbalimbali katika jamii.

“ Katika kipindi cha miaka miwili kuanzia 2021/22 hadi 2022/23), Chuo kimedahili wanafunzi 1,727 katika ngazi ya Shahada (Degree), na 3,360 kwa ngazi ya stashahada (Diploma).

Mwaka 2021/22, Chuo kilitoa jumla ya wahitimu wapatao 133 wa ngazi ya Shahada, 269 wa ngazi ya Stashahada, na 62 wa ngazi ya Cheti. Wataalamu hawa pamoja na wengine ambao wamekuwa wakizalishwa na chuo hiki wamekuwa msaada mkubwa katika utekelezaji wa miradi ya maji na sekta nyingine mtambuka” Dkt. Karia Amesema

Amesema ili kuendelea kuzalisha wataalamu wabobezi zaidi Chuo cha Maji kimeanzisha Shahada mbili za Uzamili (Masters Degree programs) ambazo zitaanza kutolewa mwaka 2023/24, Shahada hizo ni Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Rasilimali Maji na Huduma (Master Degree in Water Resources and Utility Management) pamoja na Shahada ya Uzamili ya Uhandisi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira (Master Degree in Water Supply and Sanitation Engineering)

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) akiongea katika kikao hicho ameihakikishia kamati ya Bunge kuendelea kusimamia maagizo yote yanayotolewa ili chuo kiwe mfano bora katika vyuo barani Afrika.



Chuo cha Maji kilianzishwa mwaka 1974 kama kitengo ndani ya Wizara ya Maji ambapo kimechangia kuzalisha nguvu ya rasilimaliwatu inayotumika katika Sekta ya Maji hapa nchini na nje ya nchi.



# DAWASA yaimarisha huduma ya majisafi kwa wakazi wa wilaya mbili kwa mpigo Dar

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA) imeondosha adha ya huduma ya majisafi kwa baadhi ya wakazi wa wilaya ya Kinondoni na Ubungo ambao hawakuwa na huduma ya majisafi ya uhakika jijini Dar es salaam.

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi(Mb) ameshuhudia hayo kwa kukagua utekelezaji wa mradi wa maji wa uboreshaji upatikanaji na usambazaji wa majisafi unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA) katika maeneo ya Wazo Hill, Tegeta A na Goba.

Mhe. Mahundi amewataka Mameneja wa DAWASA kanda za Mivumoni, Makongo na Kawe waendelea kwa kasi kufanya kazi ya kuunganishia wateja mbalimbali waliokamilisha taratibu ili kupata huduma ya majisafi katika makazi yao.

Mkurugenzi wa Miradi wa DAWASA Mhandisi Ramadhani Mtindasi katika ukaguzi huo amesema kuwa mradi huo unanufaisha zaidi ya makazi 15,224 yaliyopo katika maeneo ya wilaya ya Kinondoni, mitaa ya Wazo Hill, Nyakasangwe, Kisanga, Mivumoni ,Kizudi, Madale, Mbopo na Mbezi juu na Wilaya ya Ubungo mitaa ya Tegeta A, Matosa, Goba na Kulangwa.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe. Saad Mtambuli ameipongeza Serikali na Sekta ya Maji kwa ujumla kwa utekelezaji wa mradi huo ambao umeweza kuondosha changamoto ya huduma ya majisafi katika maeneo ya Wazo, Nyakasangwe, Kisanga, Mivumoni, Kizudi, Madale, Mbopo na Mbezi juu







# Ziara ya Waziri wa Maji Aweso Mkoa wa Tabora





Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ameweka jiwe la msingi la mradi wa maji wa Mji wa Kaliua ambao thamani yake ikiwa ni zaidi ya shilingi milioni 503, ujenzi wake umefika asilimia 93 na kuanza kutoa huduma ya majisafi kwa wananchi.

Mradi huo pamoja na kazi nyingine, umehusisha ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa lita 50,000 ujenzi wa raiser yenye urefu wa mita 12 na ulazaji wa bomba zenye urefu wa km 13.5

Mradi huu ni suluhisho la huduma ya majisafi kwa wananchi wakati mradi mkubwa utakaotumia maji ya ziwa Victoria ukiendelea kutekelezwa.

Wananchi wa halmashauri ya wilaya ya Kaliua wamepongeza kazi inayofanywa na Serikali katika juhudi za Serikali ya awamu sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa majibu ya changamoto ya huduma ya maji kwa wakati. Mkandarasi wa mradi wa miji 28 ameshakabishiwa na Serikali eneo la ujenzi wa mradi wilayani Kaliua.

# Maelekezo ya Rais Samia yakamilishwa Ngara ndani ya miezi 17



Hatimaye baada ya miezi 17 Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amezindua mradi wa maji wa Ngara baada ya kuelekezwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumaliza changamoto ya huduma ya majisafi mjini Ngara.

Mhe. Rais Samia alitoa maelekezo hayo tarehe 22 Februari, 2022 akiwa wilayani Ngara katika sherehe za maadhimisho ya miaka 25 ya uaskofu wa askofu Severini Niwemugizi wa jimbo la Rulenge, Ngara mkoani Kagera.

Mradi huo wa Ngara unahudumia zaidi ya wakazi elfu 18 na viongozi na wananchi wa Wilaya ya Ngara wametoa Shukrani zao za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanikisha huduma ya majisafi katika kipindi kifupi, na kuondosha changamoto iliyokuwa inawakabili kwa muda mrefu.





# Mradi wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe watakiwa kuongeza kasi




Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Prof. Jamal Katundu amekagua ujenzi wa mradi wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe na kuwataka wakandarasi kukamilisha kazi hiyo mapema ili wananchi wanaotarajia kunufaika kupata huduma ya maji waipate mapema katika maeneo ya Same na Mwanga.

Prof. Jamal katika ukaguzi huo ameridhishwa na kasi ya utekelezaji wa mradi ambao utatua changamoto ya muda mrefu za upatikanaji wa maji kwa wananchi.

Amesisitiza umuhimu wa kuzingatia ratiba ya utekelezaji wa mradi na ikiwezekana kazi ifanyike na kukamilika kabla ya muda uliopangwa kwasababu huduma ya maji ni haki ya msingi na Serikali imejipanga kufanikisha jambo hilo kwa wananchi.
Kiongozi wa Timu ya Uratibu wa Mradi Mhandisi Abbas Pyarali, amesema hadi tarehe 31 Agosti 2023 utekelezaji wa mradi huo ulikuwa umefika asilimia 79.5.





# Naibu Waziri wa Maji awataka wataalamu kufanya tafiti zenye kutoa matokeo Chanya



Naibu Waziri wa Maji, Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amewataka wataalamu wanapofanya tafiti mbalimbali ziwe suluhu katika maisha na zitumike kutoa matokeo ya majibu kwa jamii kuhusu changamoto mbalimbali, na sio kuziweka kabatini.

Mhe. Mahundi kasema hayo wakati wa kufunga Kongamano la Utekelezaji wa Programu ya Uwekezaji katika Sekta ya Maji Zanzibar.



# Nyasa -Kata nne zaambiwa zikae mkao wa kula

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amewaambia wakazi wa kata nne wilayani Nyasa kukaa mkao wa kula kwa sababu Serikali imeshajipamga kuwafikishia huduma ya majisafi.

Amezitaja kata hizo kuwa ni Mpepo, Mipotopoto, Lumeme na Uhuru ambapo Serikali itatekeleza miradi ya maji.
Mhandisi Mahundi ameainisha kuwa katika kata ya Lumeme (kijiji cha Mbanga) kwa mwaka wa fedha 2023/24 jumla ya fedha cha shilingi milioni 224 kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji, ambapo vijiji vingine vitapata huduma ya majisafi kupitia kwenye miradi itakayotekelezwa na Serikali inaendelea kutafuta vyanzo vya maji vya uhakika ambavyo vitatumika wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo.

Naye Mbunge wa Jimbo la Nyasa Mhe. Mhandisi Stella Manyanya ameishukuru Wizara ya Maji kwa kuendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji katika Jimbo la Nyasa, na kuiomba Serikali kutekeleza zaidi miradi ya maji kwa wananchi.





# Tanzania ni bora kati ya nchi 40 Ulimwenguni, Programu ya Uendelevu Huduma ya Maji



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema Sekta ya Maji katika kutekeleza Programu ya Uendelevu wa Huduma y aMaji (Pfor) hapa nchini awali ilipata dola Marekani milioni 350 na katika miaka mitatu ilifanikiwa kufikisha huduma kwa zaidi ya wananchi milioni 4.7 vijijini.
Amesema utekelezaji huo umewezesha zaidi ya watu milioni sita kuwa na vyoo bora maeneo ya vijijini katika mikoa 17.
Mhe. Aweso amesema hayo katika mafunzo ya Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa Tanzania Bara yanayoratibiwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI na Taasisi ya Uongozi, Kibaha na kuongeza hayo ni matokeo makubwa kati ya nchi 40 zinazotekeleza program hiyo kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB).
Amesema matokeo hayo makubwa yaliyopatikana Tanzania yameisukuma Benki ya Dunia kuiongezea Tanzania fedha kiasi cha dola za Marekani milioni 300, na hivyo programu ya PforR inatekelezwa katika mikoa 25 .
Waziri Aweso amewaomba Wakuu wa Mikoa kuipa ushirikiano Sekta ya Maji katika kuendeleza kazi nzuri ambapo tayari kiasi cha shillingi milioni 970 kimepelekwa katika halmashauri 52 katika mikoa nane ambayo ilikuwa hainufaiki awali.
Sekta ya Maji kupitia programu ya PforR imefanikisha zaidi ya miradi ya maji 1,500 ambayo inatoa huduma kwa wananchi.

# Mabadiliko yafanyika Sehemu ya Uchimbaji na Ujenzi wa Mabwawa kuongeza tija

Waziri wa Maji Mh. Jumaa Aweso (Mb) amebadili uongozi katika Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Sehemu ya Uchimbaji na Ujenzi wa Mabwawa,
Mabadiliko hayo yametangazwa katika kikao kilichowakutanisha watumishi wa sehemu ya Uchimbaji na Ujenzi wa Mabwawa na Chuo cha Maji, jijini Dar es salaam. Mabadiliko yanahusu Meneja wa Sehemu ya Uchimbaji na Ujenzi wa Mabwawa ambayo kwa sasa itaongozwa na Mhandisi Mashaka Sita anayechukua nafasi ya Mhandisi Simon Ngonyani.

Waziri Aweso amesema mitambo ya kisasa iliyonunuliwa na Serikali ya uchimbaji na ujenzi wa mabwawa inatakiwa ionyeshe matokeo zaidi na mabadiliko hayo yamelenga kuongeza ufanisi.





# Ruvuma

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amewahakikishia huduma ya majisafi na salama wakazi wa vijiji vya Kisuka, Lipokela na Lipanya mkoani Ruvuma kabla ya Desemba 2023.

Mhe. Mahundi amesema hayo akiwa katika ziara ya kikazi ya Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayofanyika mkoani Ruvuma.

Mhe. Mahundi pia amesisitiza kuanza kwa ujenzi wa mradi wa maji wa Matomondo ambao usanifu wake umekamilika.

Ameeleza Serikali inaimarisha huduma ya maji katika Manispaa ya Songea kwa kuanza utekelezaji wa mradi wa maji wa miji 28 ambapo kwa eneo la Songea mkataba umesha-sainiwa ukiwa na thamani ya shilingi bilioni 145.7





# TANO za Mwenge mradi wa maji wa Oldonyosambu

Mwenge wa Uhuru umeweka jiwe la msingi katika mradi wa maji wa Oldonyosambu. Mradi huo uliibuliwa mwaka 2020 kutokana na changamoto ya maji yanayotumika kuwa na madini mengi ya floride ambayo madhara yana madhara kwa afya ya binadamu.

Mradi umetekelezwa kwa kutumia fedha za ndani kupitia utaratibu wa wataalamu wa ndani wa Sekta ya Maji (Force Account) na mpaka kukamilika utagharimu shilingi 6,382,532,295.20. Hivi sasa utekelezaji upo asilimia 30 na umeshatumia kiasi cha shilingi 1,311,250,147.3.

Mradi utazalisha maji kiasi cha lita 1,036,800 ambazo zitahudumia wakazi zaidi ya 29,449 wa maeneo ya Oldonyosambu, Lemanda, Oldonyowas na Lesinoni.

Abdala Shaib Kaim, Kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa 2023 amekagua ujenzi na nyaraka za mradi huo ambapo ameridhika na utekelezaji unaoendelea. Ameridhika viwango na ubora wa ujenzi ikiwa ni pamoja na thamani ya fedha kuakisi matokeo na ubora wa mradi.

Amesema nyaraka ziko vizuri na kupongeza kuwepo kwa cheti cha tathmini ya athari za mazingira na kusisitiza mradi ukamilike kwa wakati kwa kuwa maji ni hitaji la muhimu, pia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha ( AUWSA) kuhakikisha inawasambazia wananchi maji majumbani na kwa ambao hawana uwezo wa kugharamia kupelekewa maji nyumbani wasogezewe huduma karibu katika vituo vya umma vya kuchota maji, kwasababu dhamira ya Serikali inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma ya majisafi na salama.





# Naibu Waziri Mhandisi Mahundi awaagiza DUWASA kufikisha maji Zahanati ya Ntyuka




Naibu Waziri wa Maji Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amemuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) Mhandisi Aron Joseph kuhakikisha anafikisha huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza kwenye zahanati ya Ntyuka, kata ya Ntyuka Jijini Dodoma. Agizo hilo amelitoa wakati akizindua mradi wa maji wa Ntyuka-Chimalaa kwa niaba ya Waziri wa Maji. Mradi huo umetekelezwa kwa gharama ya shilingi Milioni 471.8

Amesema dhamira ya serikali ni kuhakikisha inamtua mama ndoo ya maji kichwani huku ikifikisha huduma ya majisafi na salama katika maeneo yote ya huduma za kijamii. Kwa maana hiyo Mkurugenzi ahakikishe Zahanati hiyo iliyoko katika eneo la mradi inafikishiwa huduma ya maji haraka iwekanavyo. Amewahakikishia wananchi wa jiji la Dodoma na Tanzania kwa ujumla kuwa serikali itaendelea na jitihada zake za kuhakikisha huduma za kijamii zinafikiwa na huduma ya majisafi na salama.

Aidha, amewapongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa mazingira Dodoma kwa kusimamia vizuri hadi kukamilika kwa mradi huo.

Akitoa taarifa ya mradi huo Mhandisi Aron amesema umetekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza imekamilika na inahudumia wakazi wapatao 1,931 katika maeneo ya Ntyuka mtaa wa Chimalaa. Awamu ya pili inatarajiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/24 na itanufaisha wakazi wapatao 2,510 wa mtaa wa Nyerere na hivyo kufanya jumla ya wanufaika wa mradi huo kufikia 4,441.

# MWAUWASA yafikisha asilimia 81 ya upatikanaji majisafi Nansio

Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Mhe. Hassan Bomboko ameipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) kwa jitihada zake za kufikisha huduma ya majisafi na salama kwa wananchi wa mji mdogo wa Nansio wilayani humo.

Mhe. Hassan Bomboko ametoa pongezi hizo wakati wa ziara ya kukagua chanzo cha maji cha Nebuye ili kujionea hali halisi ya ufanisi wake.

"Nimepokea taarifa ya utekelezaji wa usambazaji maji katika mji wa Nansio, niwapongeze MWAUWASA kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji ni ya uhakika"Mhe. Bomboka amesema na kuwaasa wananchi kulinda na kutunza miundombinu ya maji sambamba na kulipa ankara za maji kwa wakati ili kuwa na huduma endelevu.

"Ni muhimu kutunza vyanzo vyetu na miundombinu ya maji kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyowekwa.
Ninawaelekeza wavuvi kuacha mara moja kufanya shughuli za uvuvi jirani na dakio la maji ili kuepusha uchafuzi wa maji yanayofikishwa kwa wananchi" Mhe. Bomboka amesema.

Meneja wa MWAUWASA Kanda ya Nansio, Mhandisi Edward Joseph amefafanua kuwa MWAUWASA inahudumia kata nane za Bukongo, Nkilizya, Kagera, Kakerege, Bukindo (kijiji cha Bulamba), Nakatunguru, Nansio (Namagubo A na B) na Namagondo (Malegeya) ambazo ni sawa na vijiji 11 kati ya vijiji 12.

Chanzo cha maji cha Nebuye kinazalisha lita milioni 8.6 kwa siku zinazohudumia wananchi zaidi ya elfu 68 ambayo ni sawa na asilimia 81 ya wananchi wanaopata huduma ya maji Nansio..

Mhandisi Edward Joseph amesema kituo cha kuzalisha maji cha Nebuye kwa sasa kina miundombinu ya matenki ya kuhifadhi majisafi kupitia tenki la Malegeya lenye uwezo wa kuhifadhi lita 3,000,000 na Nebuye lenye uwezo wa kuhifadhi lita 350,000 pamoja na sehemu maalumu ya kutupa takangumu la Hamkoko.

Kwa sasa mpango uliopo ni kuongeza mtandao maeneo ambayo bado hayajafikiwa na huduma ambayo ni sawa na takribani kilometa 68. Hatua hii itaongeza idadi ya maunganisho ya maji kutoka 4,000 hadi 10,000 ifikapo Juni 2030

Mji wa Nansio ni miongoni miji midogo ya ukanda wa Ziwa Victoria inayohudumiwa na MWAUWASA mingine ni Misungwi, Magu na Ngudu. MWAUWASA vilevile inahudumia Wilaya za Nyamagana na Ilemela.










# Aweso akunwa Uvinza na Teknolojia ya matanki ya Maji

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amekagua mradi wa maji wa vijiji vya Mlela na Kandaga uliopo kata ya Kandaga Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma wenye thamani ya shilingi 896,634,902 na kusifu teknolojia ya tanki lililotumika la Weholite, linalochukua ujazo wa lita 300,000. Tanki hilo limechukua gharama ndogo na muda mfupi ikilinganishwa na ujenzi wa matanki kwa kutumia zege.

"Nimefarijika sana baada ya kutembelea na kukagua mradi wa Maji wa vijiji vya Mlela na Kandaga, kata ya Kandaga na kujionea ubunifu wa teknolojia ya matanki ya Weholite inavyoweza kurahisisha utekelezaji wa miradi ya Maji kwa gharama nafuu na muda mfupi" Waziri Aweso amesema.

Ameongeza kuwa mradi huo wa kutumia matenki hayo ni matokeo ya kikao alichofanya baada ya kuteuliwa na kampuni zinazozalisha bidhaa mbalimbali zinazotumika katika miradi ya maji na kushauri ubunifu wa matenki ambayo yatarahisishia kupeleka huduma kwa wananchi kwa haraka na kwa gharama nafuu.

Nao wakazi na wananchi wa eneo hilo wamemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kupata mradi huo ambao umetatua adha ya maji katika makazi yao na vijiji hivyo.







Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiwa Uvinza na kujionea teknolojia rahisi ya ujenzi wa matenki ya maji

# Aweso aridhishwa na ujenzi wa jengo la Wizara ya Maji



Waziri wa Maji Mhe Jumaa Aweso (Mb) amekagua na kuridhishwa na kasi ya maendeleo ya ujenzi wa jengo la Wizara ya Maji katika Mji wa Serikali, Mtumba Jijini Dodoma.
"Nitumie nafasi hii kumshukuru Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha zaidi ya shilingi billioni 22.9 kwa ajili ya ujenzi wa jengo hili na kupata mazingira mazuri kwa watumishi wetu wa Wizara ya Maji." Mhe. Aweso amesema



Ameongeza kuwa ujenzi wa jengo hilo umefika asilimia 96 na lina uwezo wa kuhudumia watu zaidi ya 518 hivyo ni jambo kubwa na lenye kuleta tija na ufanisi kwa watumishi wa Sekta ya Maji.

Waziri Aweso amewapongeza wataalamu wa Wizara ya Maji wanaosimamia kazi hiyo na Mkandarasi kwa sababu Wizara imeridhika kwa kasi na viwango vya ujenzi.
Waziri Aweso amemuelekeza mkandarasi kuzingatia muda wa mkataba.

# Maandalizi ya Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara, Idara za Umma na Ofisi za Mikoa -SHIMIWI mwaka 2023, Timu ya Maji yapigwa jeki






Benki ya Biashara Tanzania (Tanzania Commercial Bank) Kanda ya Kati, Dodoma leo imekabidhi vifaa vya michezo kwa timu ya Wizara ya Maji ikiwa ni sehemu ya kuuunga mkono jitihada za serikali katika kuhamasisha na kuinua Michezo kwa Watumishi wa Umma.
Meneja wa Benki hiyo Kanda ya Kati, Dodoma Shabani Telatela akikabidhi vifaa hivyo kwa uongozi wa Wizara ya Maji, ameshukuru kwa ushirikiano mkubwa uliopo katika kuwafikishia huduma wananchi kwa uongozi wa Wizara ya Maji.

Vifaa hivyo, vimepokelewa na Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Rasilimali Watu Bi. Wanyenda Kutta kwa niaba ya Katibu Mkuu, Wizara ya Maji ambapo ameishukuru Benki hiyo kwa vifaa hivyo na kuahidi Maji itaibuka kinara katika mashindano hayo.

# Mradi wa maji wa miji 28, Kazi kwa vitendo Songea Bilioni 145.77 za Rais Samia zinatumika







Timu ya Wataalamu kutoka Wizara ya Maji, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA) na Halmashauri ya Manispaa ya Songea imetembelea maeneo ambayo mradi wa Maji wa Miji 28 utatekelezwa na kufanya mikutano na wananchi ili kuwajengea uelewa wa pamoja wa mradi na kuwataarifu kuhusu kuanza kwa utekelezaji wake.

Timu hiyo ya wataalamu imetembela na kukagua eneo ambalo mkandarasi amejenga kambi kwa ajili ya kuanza kutekeleza kazi hiyo.

Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi ambaye ni kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) na thamani yake ni shilingi bilioni 145.77

Wananchi wamepokea kwa furaha kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo na wameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutenga fedha za ujenzi wa mradi wa maji wa Miji 28 kwa kuwa utakuwa na manufaa makubwa kwa wakazi wa Mji wa Songea.

# Nandagala A na B mambo safii





Naibu Waziri wa Maji , Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) ameambatana na Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Taifa Ndugu Mary Chatanda katika ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Ziara hiyo imewafikisha katika mradi wa maji wa uboreshaji huduma ya maji vijiji vya Nandagala A & B uliopo Wilaya ya Ruagwa ambapo wananchi wameanza kunufaika ingawa mradi utekelezaji wake ni asilimia 90. Miradi hii inatekelezwa kwa gharama ya shilingi 1,607,102,414.12.

Mhe. Mahundi katika ziara hiyo ameeleza dhamira ya Serikali inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu "Kumtua mama ndoo ya maji kichwani" kwa vitendo. Wilaya ya Ruagwa kwa mwaka fedha 2023/24, Serikali inatekeleza mradi mkubwa wa maji kwa kutumia chanzo cha Mto Nyangao ambapo Mkandarasi wa ujenzi ameshalipwa malipo ya awali ili aanze utekelezaji.

# " Maadili ya viongozi ni msingi muhimu" Mahundi

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amesema maadili ya viongozi ni msingi muhimu kwa uongozi bora na wenye tija kwa maendeleo endelevu.

Mhe. Mahundi (Mb) amesema hayo kwa niaba ya Waziri wa Maji, wakati akifungua mafunzo elekezi kwa bodi ya wakurugenzi ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), mkoani Iringa Amesema mafunzo hayo yatawapa RUWASA mwanga na kuwaimarisha katika kuongoza kwa mfano na kuendeleza maadili katika kutekeleza majukumu.

Mhe. Mahundi amewataka wajumbe wa bodi kupitia mafunzo hayo kupata ufahamu wa viashiria hatarishi hivyo kuweza kutambua na kupunguza viashiria hivyo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya RUWASA Mhandisi Ruth Koya ameishukuru Wizara ya Maji kwa ushirikiano mzuri wakati wa utekelezaji wa majukumu yake katika kufanikisha lengo la Serikali la kutoa huduma ya majisafi kwa wananchi.

# Kilolo: Uhambingeto sasa safii



Mradi wa maji wa Uhambigeto uliopo Kilolo mkoani iringa hivi sasa umeanza kutoa huduma ya majisafi kwa wananchi na kuondosha adha iliyokuwa ikiwapata kuhusu maji.

Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Menejimenti pamoja na watumishi wa RUWASA Mkoani Iringa wamekagua mradi huo ambao unatakiwa kukamilika ifikapo Septemba 2023.

Hata hivyo, tayari wananchi wa maeneo hayo wameanza kupata huduma ya maji huku mradi ukiwa katika hatua za mwisho za utekelezaji.

Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi RUWASA Mhandisi Ruth Koya amefurahishwa na uchapakikazi wa wataalamu wa RUWASA hivyo kuweka tumaini kuwa kazi hiyo itakamilika kabla ya tarehe 30 Septemba, 2023 furaha na ubora wa kazi umemfanya

Mhandisi Koya kuwapa mafundi shilingi 157,000 kama motisha kwa kazi nzuri.

Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Ndugu Daniel Chongolo alielekeza mradi huo ufanyiwe kazi na kutoa huduma kwa wananchi mapema.



Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amesema mradi wa maji wa Shemwengo, katika kata ya Inyala mkoani Mbeya utatekelezwa kwa thamani ya shilingi milioni 458.7.

Amesema hayo wakati wa ziara ya Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mkoani Mbeya







Naibu Waziri wa Maji, Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amekagua utekelezaji wa miradi ya maji katika wilaya ya Mafia. Miradi hiyo ni mradi wa maji wa Jibondo, na Kilindoni, pia amezindua mradi wa maji wa Jimbo (Kidika).

Amewataka wataalamu wa Sekta ya Maji wa Mafia kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji kwa weledi katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi na salama katika makazi yao, pia amewataka Wakandarasi kukamilisha miradi ya maji kuendana na mkataba.



Katibu Mkuu Wizara ya Maji Prof. Jamal Katundu amefanya ziara ya kikazi katika Mji wa Monduli ili kujionea hali ya huduma ya upatikanaji wa huduma ya majisafi.

Ametembelea kituo cha kusuma maji cha Ngaramtoni ambapo hivi sasa Pampu moja imeshafungwa na pampu ya pili itafika nchini tarehe 15 Septemba 2023, na pia ametembelea matanki ya maji ya Monduli.

Prof. Jamal ameitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha ( AUWSA) kuhakikisha inafunga pampu ya pili kwa wakati na kuimarisha huduma ya maji ikiwa ni pamoja na kutumia magari ya majisafi (water bowser) ili kuweza kuondoa adha ya majisafi katika maeneo ambayo huduma bado haijaimarika.











Katibu Mkuu Wizara ya Maji Prof. Jamal Katundu amekagua Mradi wa majisafi wa Dareda -Singu-Sigino-Bagara ulioko Wilayani Babati mkoani Manyara na kuwaagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati (BAWASA) kukamilisha Mradi huo kabla ya tarehe 30 Septemba, 2023.

Mradi umefika asilimia 95 ya utekekezaji na amesema serikali itatoa shilingi milioni 224 ndani ya siku tatu kwa ajili ya kukamilisha Mradi.

Mkurugenzi Mtendaji wa BAWASA , Mhandisi Iddy Msuya amemshukuru Katibu Mkuu na kumhakikisha kuwa Mradi huo utakamilika ndani ya muda alioagiza,
Pia amemshukuru Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kufuatilia kwa karibu utekekezaji wa mradi huo na kuhakikisha fedha zinapatikana na wananchi wa Kata za Sigino,Dareda na Bagara wanapata huduma ya majisafi na salama.

# KAHAMA: Mtuhumiwa wa wizi wa maji ashikwa katika bustani yake



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama (KUWASA) imewataka wananchi wanaofanya kazi ya kulima bustani za mbogamboga kuacha utamaduni wa kuhujumu miundombinu ya usambazaji wa majisafi kwa wananchi.

Wananchi hao wametakiwa kufuata taratibu za kuomba kuunganishiwa huduma ya maji katika maeneo yao ili kukidhi mahitaji ya kufanikisha shughuli hiyo ya kilimo cha bustani za mboga.

Afisa Uhusiano wa Mamlaka ya Maji Kahama (KUWASA) John Mkama amesema hayo baada ya kumkamata mkulima wa bustani ya mboga mboga Averina William ambaye anatuhumiwa kujipatia maji kinyume na utaratibu kwa ajili ya kumwagilia bustani katika eneo la Nyasubi.
Mkama amesema kitendo hicho kinasababisha hasara kwa KUWASA na kuzorotesha huduma ya majisafi kwa wateja.

Mtendaji wa Kata ya Nyasubi Innocent Kapere amesema kilimo hicho kinawasaidia wananchi kwa kipato na matumizi ya nyumbani, ila njia wanayotumia ya kupata maji ya kumwagilia bustani ni kinyume na utaratibu wa Serikali.
Mmiliki wa bomba la maji lililokatwa Daniel Yazidi amesema bomba hilo limekuwa likikatwa maksudi kwa minajili ya kufanisha umwagiliaji katika bustani za mboga mboga.
KUWASA inawashukuru wananchi wote wanaowafichua waharibifu wa miundombinu ya usambazaji majisafi kwa umma na itaendelea kutoa motisha kwa wote wanaotoa ushirikiano katika kufuchua uharibifu huo.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kigoma (KUWASA) imekabidhiwa gari ili kuimarisha utendaji wa kazi na kuhudumia wananchi.

KUWASA imekabidhiwa gari na Katibu Mkuu, Wizara ya Maji kufuatia maelekezo yaliyotolewa na Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) hivi karibuni mkoani Kigoma akikagua utekelezaji wa miradi ya maji na kuelekeza kuwaongezea KUWASA vitendea kazi ili kuimarisha huduma ya majisafi kwa wananchi.







# Mradi wa maji Kasulu mfano wa Sekta ya Maji - Aweso



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amekagua mradi wa maji wa Makere na kuridhishwa na utekelezaji wake, na kusema uwe somo la kujifunzia katika kutekeleza wa miradi ya Sekta ya Maji.



Mradi unanufaisha vijiji vitatu vya Makere, Kalimungoma na Nyangwa, ambapo ujenzi wake umekamilika na unatoa huduma ya majisafi kwa zaidi ya wakazi 30,293.

Mradi huu umefanikishwa kwa ufadhili wa Shirika la Water Mission kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kugharimu kiasi cha shilingi cha shilingi 1,213,209,200.
Kazi zilizotekelezwa ni Pamoja na ujenzi wa tanki la lita 200,000, ujenzi wa magati 36 , ujenzi wa nyumba ya mitambo na kutibu maji maji, ufungaji wa mitambo ya kutibu maji, ufungaji wa sola paneli 98, ufungaji wa pampu, ulazaji wa bomba mita 14,667 na uchimbaji wa kisima kirefu.

Mbunge wa Kasulu vijijini Mhe Augustine Vuma Hole ameishukuru Serikali pamoja na Shirika la Water Mission kwa kuhakikisha mradi unajengwa na kukamilika na kuwaondolea adha wananchi ya upatikanaji wa huduma ya maji.

Waziri Aweso ameridhiridhishwa na ujenzi wa mradi na kumshukuru Mh. Dkt.Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri na kufungua milango kwa wafadhili kujitokeza na kushirikiana na Serikali kutekeleza ujenzi wa miradi ya maji kufanikisha azma ya "kumtua mama ndoo kichwani".

# Kakonko sasa safiii

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amekagua na kuzindua mradi wa maji wa Chilambo Wilaya ya Kakonko mkoani Kigoma.

Mradi huo unanufaisha zaidi ya wakazi 3,500. Kakonko ni wilaya iliyokuwa na changamoto ya huduma ya maji.

Mhe. Aweso ameshuhudia mageuzi makubwa katika Sekta ya Maji wilayani hapo, ambapo gharama ya mradi huo ni shilingi 873,790,739.13
Akiongea na wananchi amewataka kutunza mradi huo, Pamoja na miundombinu yake ili huduma yam aji iwe endelevu.







# Mwitikio wa Kauli ya Waziri Aweso, Mipaka yaimarishwa Hifadhi ya Makutopora




Maelekezo ya Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) kuhusu kuhifadhi na kuendeleza vyanzo vya maji hapa nchini kwa kuwashirikisha viongozi na wananchi yameshika kasi na kufanikishwa katika eneo la hifadhi ya Makutopora, Jijini Dodoma.

Waziri Aweso alitoa maelekezo hayo hivi karibuni katika kikao kazi na watendaji wa Sekta ya Maji ambapo alisisitiza ili huduma ya maji iwe endelevu upo umuhimu wa dhati kwa kila kiogozi na wananchi kushirikishwa katika kazi ya uhifadhi.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mhe. Jabbir Shekimweri, kufuatia hilo ametembelea eneo la hifadhi ya maji chini ardhi - Makutopora na kukagua utekelezaji wa maagizo ya shughuli za uhifadhi wa eneo hilo zinazoendelea.
Mhe. Shekimweri amekagua njia zilizochongwa kwa ajili ya kuzuia adhari za moto zenye urefu wa kilometa 22, alama za mipaka kuonyesha mwanzo wa hifadhi na mwisho wa hifadhi pamoja na kukagua alama za kudumu za mipaka (beacon).

Mhe. Shekimweri ameridhishwa na utendaji kazi uliofanyika ikiwamo ujenzi wa alama za kudumu zenye ukubwa wa mita mbilizinazoonekana jambo litakalosaidia kupunguza uvamizi kwa visingizio vya kutokufahamu eneo ni la hifadhi. Kamati ya ulinzi na usalama ya Wilaya ya Dodoma imetoa pongezi kwa ubunifu wa njia zilizochongwa kwasababu zimekidhi viwango vya uzuiaji wa moto hivyo kero za moto kushambulia eneo kubwa zitapungua.







**Kitengo cha Mawasiliano**

Tovuti: www.maji.go.tz